

HABARILEO 19th JULY 2018

Mwanafunzi azindua taulo za kike za 'kudumu'

Na Lucy Ngowi

MWANAFUNZI Zyaan Virji (16) amezindua taulo za kike zinazoweza kutumika kwa miaka mitatu hadi mitano, lengo likiwa ni kuwarahisishia wasichana wasio na uwezo, kuzitumia wanapokuwa kwenye hedhi.

Virji ambaye ni kijana wa kiume, ambaye pia ni mwanafunzi katika Shule ya Aga Khan, alisema sababu

zilizomsukuma kutoa taulo hizo, ni kwa kuwa taulo nyingine za kike zinazawa bei kubwa, hali inayowawia vigumu wale wenye kipato cha chini.

Alisema aligundua idadi kubwa ya wanawake wanaoishi maeneo ya vijijini wamekuwa wakipata shida wakati wa kipindi cha hedhi hasa kwa wanafunzi, ambao baadhi yao wamekuwa wakishindwa kuhudhuria masomo kutokana na hali hiyo jambo linalowafanya

kupoteza haki zao za msingi za kuhudhuria masomo.

"Siku moja katika pitapita zangu madukani nikaona moja kati ya bidhaa za hedhi ikiuzwa kwa bei ghali sana, nikajikuta nikiingwiwa na maswali mengi, ni nini ambacho kinafanya taulo hizi kuuzwa ghali hivi?"

Hivi wasichana na wanawake wenye hali ngumu wataweza kumudu, kama tu baadhi yao wanashindwa kujikimu kwa mlo wa kila siku watawezaje kutoa fedha

kwa ajili ya kujinunulia taulo za kike?" alihoji.

Alisema taulo hizo zitauzwa kwa Sh 12,000 hadi 15,000 ambapo mnunuaaji atajipatia sabuni pamoja taulo za kike nane na atakapomaliza anaweza kuzisafisha na kurudia tena kuzitumia.

Naibu Waziri wa zamani wa Maendeleo ya Jamii, Wanawake, Jinsia na Watoto, Shamim Khan, alimpongeza Virji kwa kubuni kitu kama hicho na kuwataka vijana wengine kuiga mfano huo.